Arusha, Tanzania
Tovuti: www.african-court.org
Simu: +255-27-970-430

**MUHTASARI WA HUKUMU**

**UMALO MUSSA DHIDI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAOMBI NA. 031/2016**

**HUKUMU KUHUSU HOJA ZA MSINGI NA FIDIA**

**13 JUNI 2023**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU**

**Arusha, tarehe 13 Juni 2023**: Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu (Mahakama) ilitoa hukumu katika kesi ya Umalo Mussa dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Bwana Umalo Mussa (Mwombaji) ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye, wakati wa kuwasilisha Maombi haya, alikuwa gerezani akisubiri kunyongwa kufuatia kutiwa hatiani kwa kosa la mauaji. Mwombaji alidai kuwa Nchi Inayolalamikiwa ilikiuka haki zake zinazolindwa chini ya Ibara ya 7(1)(a), (c) na (d) ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu (Mkataba) kwa kumtia hatiani kwa msingi wa maelezo yake ya kujitia hatiani ambayo aliyakataa, kwa kutompa wakili wa chaguo lake na kwa madai ya kuchelewesha kusikilizwa na uamuzi wa maombi yake ya mapitio, mtawalia. Aliomba fidia kutokana na madai ya ukiukwaji huo, kwamba alipwe fidia kwa muda wa kifungo chake na atolewe gerezani.

Nchi Inayolalamikiwa iliwasilisha pingamizi dhidi ya mamlaka ya Mahakama hii. Ilidai kuwa Mwombaji anaiomba Mahakama kuketi kama mahakama ya rufaa na kuamua masuala ambayo yameamuliwa na Mahakama yake ya Rufani, hususani kupokelewa kwa maelezo ya ziada yaliyotolewa nje ya mahakama kama ushahidi. Pia, Nchi Inayolalamikiwa ilidai kuwa Mahakama hii haina mamlaka ya kutengua hukumu hiyo, kutengua adhabu na kumwachia Mwombaji kutoka gerezani. Nchi Inayolalamikiwa pia ilibainisha kwamba Maombi hayaoneshi suala lolote kuhusu tafsiri ya Mkataba, Protokali ya Mkataba, kuhusu Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu (Protokali) au hati zozote za haki za binadamu zilizoridhiwa na Nchi Inayolalamikiwa. Badala yake, yanaibua masuala ya kisheria na ushahidi ambayo yalishughulikiwa na mahakama za ndani.

Kuhusu hoja ya kwanza ya pingamizi hilo, Mahakama iliamua kwamba haitakaa kama mahakama ya rufaa wala kupitia ushahidi uliotolewa katika Mahakama ya Rufani ya Tanzania ili kufanya tathmini ya mashauri ya ndani yaliyosababisha Mwombaji kutiwa hatiani na kuhukumiwa kinyume na sheria na

viwango vilivyowekwa katika Mkataba au hati nyingine za haki za binadamu zilizoridhiwa na Nchi Inayolalamikiwa. Kuhusu hoja ya pili, kwamba Mahakama haina uwezo wa kufuta hatia na kufuta hukumu, Mahakama ilithibitisha kwamba, kwa mujibu wa Ibara ya 27(1) ya Protokali, "ikiwa itabaini kuwa kuna ukiukwaji wa haki za binadamu", inaweza "kutoa maagizo yanayofaa ili kurekebisha ukiukwaji, ikijumuisha malipo ya fidia ya haki" na haya yanaweza kuhusiana na hukumu zinazotolewa kwa mwathirika wa ukiukwaji wa haki za binadamu. Kuhusiana na hoja ya tatu, Mahakama ilirejelea masharti ya Ibara ya 7 ya Protokali na kuthibitisha kuwa itaamua masuala yanayojitokeza katika Maombi bila kujali kama Mwombaji ametaja masharti sahihi ya Mkataba na hati nyingine za haki za binadamu zilizoridhiwa na Nchi Inayolalamikiwa. Hivyo Mahakama ilibaini kuwa ina mamlaka ya kushughulikia Maombi haya.

Ingawa vipengele vingine vya mamlaka yake havikupingwa na Nchi Inayolalamikiwa, Mahakama ilivichunguza. Kwa mujibu wa mamlaka yake binafsi, Mahakama iliona kuwa ilikuwa na mamlaka ya binafsi tangu tarehe 29 Machi 2010, Nchi Inayolalamikiwa iliwasilisha Tamko lililotolewa chini ya Ibara ya 34(6) ya Protokali na Tamko hili linawaruhusu watu binafsi kuwasilisha maombi dhidi yake kama ilivyoainishwa na Ibara ya 5(3). Mahakama pia ilibaini kuwa Nchi Inayolalamikiwa uondoaji wake wa Tamko hilo tarehe 21 Novemba 2019 haukuathiri Maombi haya, kwani uondoaji huo ulianza tarehe 22 Novemba 2020, wakati Maombi haya yaliwasilishwa Mahakamani tarehe 8 Juni 2016. Mahakama pia ilisisitiza kwamba ilikuwa na mamlaka ya muda kwa sababu madai ya ukiukwaji yalikuwa yakiendelea kwa asili; na mwisho, kwamba ilikuwa na mamlaka ya eneo, ikizingatiwa kwamba tukio hilo lilitokea ndani ya eneo la Nchi Inayolalamikiwa ambayo ni Mwanachama wa Protokali.

Kuhusu kupokelewa kwa Maombi haya, Mahakama ilipitia kwanza mapingamizi mawili (2) yaliyowasilishwa na Nchi Inayolalamikiwa. Haya yalitokana na kushindwa kuzingatia masharti ya kutumia kikamilifu usuluhishi wa ndani na, kuwasilisha Maombi haya ndani ya muda stahiki baada ya kumalizika kwa usuluhishi wa ndani, kama ilivyobainishwa chini ya Ibara za 56 (5) na (6) za Mkataba na kurejelewa katika Kanuni 50(2)(e) na (f) ya Kanuni za Mahakama, mtawalia.

Katika pingamizi la kwanza, Nchi Inayolalamikiwa ilidai kuwa Maombi haya yaliwasilishwa kabla ya muda wake kwa kuwa Mwombaji alipaswa kwanza kuwasilisha shauri la kikatiba katika Mahakama Kuu ya Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 13(6) ya Katiba ya Tanzania (1977) na kuomba mapitio ya uamuzi wa Mahakama ya Rufani wa kurekebisha madai ya ukiukwaji wa haki yake ya kusikilizwa. Mahakama ilirejelea uamuzi wake wa awali katika kesi zinazohusu Nchi Inayolalamikiwa, kwamba kuwasilisha maombi ya kikatiba katika Mahakama Kuu na matumizi ya utaratibu wa mapitio katika mfumo wa mahakama wa Nchi Inayolalamikiwa ni suluhu zisizo za kawaida ambazo Mwombaji halazimiki kuzitumia

kabla ya kuifikia Mahakama hii. Kwa kuwa Mahakama ya Rufani ya Tanzania, chombo cha juu zaidi cha mahakama katika Nchi nayolalamikiwa, kwa hukumu yake ya tarehe 21 Mei 2009 kuhusu rufaa ya Mwombaji, ilikubali kutiwa hatiani kwake na adhabu yake kufuatia mashtaka ambayo alidai yalikiuka haki zake, Mahakama hii iliona kuwa Mwombaji alikuwa amemaliza suluhu za ndani kabla ya kuwasilisha Maombi haya.

Pingamizi la pili la Nchi Inayolalamikiwa lilikuwa kwamba Maombi haya hayakuwasilishwa ndani ya muda mwafaka baada ya kumalizika kwa usuluhishi wa ndani, kwani yaliwasilishwa miaka saba (7) baadaye. Mahakama hii ilitoa uamuzi kwamba Mwombaji alimaliza usuluhishi wa ndani tarehe 21 Mei 2009, wakati Mahakama ya Rufaa ilipotupilia mbali rufaa yake. Hata hivyo, ilikuwa ni baada ya tarehe 29 Machi 2010 ambapo Nchi Inayolalamikiwa iliwasilisha Tamko la kukubali mamlaka ya Mahakama chini ya Ibara ya 34(6) ya Protokali, ambapo Mwombaji aliweza kuwasilisha Maombi haya.

Kwa kawaida, kipindi kitakachozingatiwa kwenye tathmini ya muda stahiki wa kuwasilisha Maombi kitakuwa kipindi cha kati ya 29 Machi 2010, tarehe ya Nchi Inayolalamikiwa kuwasilisha Tamko, na tarehe 8 Juni 2016, tarehe ya kuwasilisha Maombi, yaani miaka sita (6), miezi miwili (2) na siku kumi na tisa (19). Mahakama pia ilisisitiza msimamo wake kwamba, ingawa utaratibu wa mapitio katika Mahakama ya Rufani ya Nchi Inayolalamikiwa ni suluhu isiyo ya kawaida ya kimahakama ambayo mwombaji halazimiki kuitumia, katika kesi ambapo walijaribu kutumia suluhu hii, Mahakama itazingatia muda huo umetumika katika kutafuta suluhu ili kubainisha kama Maombi yaliwasilishwa Mahakamani ndani ya muda mwafaka. Katika kesi hii, Mwombaji alidai kuwa tarehe 11 Machi 2014, aliwasilisha maombi ya mapitio ya uamuzi wa Mahakama ya Rufani, baada ya kupewa kibali na Mahakama ya Rufani kufanya hivyo, nje ya muda na kwamba maombi hayo yalikuwa yanasubiria uamuzi kufikia wakati alipowasilisha Maombi haya tarehe 8 Juni 2016. Nchi Inayolalamikiwa ilipinga madai haya. Mwombaji pia alishindwa kutoa ushahidi kuwa Mahakama ya Rufani ilimpa kibali cha kuwasilisha maombi ya mapitio nje ya muda na kwamba aliwasilisha maombi ya mapitio. Katika mazingira haya, Mahakama hii iliona maombi ya mapitio kuwa hayakuwasilishwa na hivyo, haikuweza kutathmini muda unaodaiwa kutumiwa na Mwombaji kutafuta suluhu ili kuamua muda stahiki wa kuwasilisha Maombi.

Hata hivyo, Mahakama ilibainisha kuwa kipindi cha kati ya mwaka 2007 na 2013 kilikuwa ni miaka ya uanzishwaji wa Mahakama na kama ilivyokuwa hapo awali, katika kipindi hicho, wananchi, hasa wale walio katika hali kama ya Mwombaji, hawakuweza kudhaniwa kuwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu uwepo wa Mahakama ili kuwasilisha maombi yao mara baada ya kumalizika kwa taratibu za ndani. Hivyo, Mahakama iliamua kwamba muda wa kutathminiwa kwa kuzingatia masharti ya kuwasilisha Maombi ndani ya muda mwafaka, ni kati ya mwaka 2013, wakati ambapo umma

ungetarajiwa kuwa na ufahamu kuhusu Mahakama, na 2016, mwaka ambao maombi yaliwasilishwa, ambapo ni kipindi cha miaka mitatu (3).

Mahakama, baada ya kuzingatia kuwa Mwombaji alikuwa amejiwakilisha mwenyewe alipowasilisha Maombi mbele ya Mahakama, akiwa kwenye orodha ya kunyongwa, akiwa ametengwa na watu kwa ujumla na kuwa kwenye vikwazo vya kutoka eneo moja hadi jingine na upatikanaji wa taarifa iliamua kwamba uwasilishaji wa Maombi haya ndani ya muda wa miaka mitatu (3) baada ya kutumia kikamilifu usuluhishi wa ndani, ulikuwa mwafaka.

Kisha Mahakama ilijiridhisha kwamba masharti mengine ya kupokelewa yaliyowekwa katika Ibara ya 56 ya Mkataba yalitimizwa. Ilisisitiza kuwa utambulisho wa Mwombaji ulibainishwa, maombi yamezingatia Sheria Anzilishi ya Umoja wa Afrika na Mkataba; na kwamba hayakuwa na lugha ya kudhalilisha wala matusi. Mahakama pia ilibaini kuwa Maombi haya hayakutokana na taarifa pekee zilizosambazwa kupitia vyombo vya habari na kwamba hayakuhusu kesi ambayo tayari zilikuwa zimesuluhishwa kwa mujibu wa Ibara ya 56 (7) ya Mkataba. Hivyo, Mahakama iliona Maombi haya yanakubalika.

Kuhusiana na hoja za msingi, Mahakama ilizingatia iwapo Nchi Inayolalamikiwa ilikiuka haki za Mwombaji chini ya Ibara ya 7(1)(a), (d) na (c) ya Mkataba. Hii ilikuwa ni kwa kuchunguza madai ya Mwombaji kuhusu madai ya ukiukwaji wa haki yake ya kusikilizwa, ukiukwaji wa haki zake kutokana na kuchelewa kusajiliwa na kuamuliwa kwa maombi yake ya mapitio na ukiukwaji wa haki yake ya kujitetea kutokana na kutopewa mawakili wa chaguo lake.

Katika madai ya kwanza ya ukiukwaji wa haki ya kusikilizwa, Mwombaji alidai kuwa (i) Mahakama Kuu ilipokea kimakosa ushahidi wa maelezo yake ya kujitia hatiani, ambayo aliyakana na (ii) Mahakama ya Rufani ilikosea kisheria na kushindwa kuzingatia utetezi wake, kwamba maelezo ya nje ya mahakama yalitolewa kwa kulazimishwa.

Mahakama ilibaini kwamba hakuna chochote katika utaratibu uliofuatwa na Mahakama Kuu, yaani, kuendesha *shauri ndani ya shauri*, ili kukubali maelezo ya Mwombaji ya kujitia hatiani kuwa ushahidi, ambacho kilionyesha kuwa haki ya Mwombaji kusikilizwa ilikiukwa. Zaidi ya hayo, Mahakama Kuu ilitupilia mbali ushahidi wa mashahidi wawili wa upande wa mashtaka ambao ulikinzana na kutegemea ushahidi wa mdomo wa shahidi mmoja tu wa upande wa mashtaka, ushahidi wa maandishi wa ripoti za kifo za marehemu na ripoti ya uchunguzi wa kitabibu wa Mwombaji ikionyesha kwamba hakuteswa. kama inavyodaiwa. Ushahidi wa maandishi ulikubaliwa kuwa ushahidi baada ya wakili wa Mwombaji kutopinga.

Katika madai ya pili ya mwombaji kuhusu madai ya makosa ya kisheria na masuala ya msingi kwenye Mahakama ya Rufani, Mahakama hii ilibainisha kuwa Mahakama ya Rufani ilithibitisha kuwa maelezo yaliyokubaliwa na Mahakama Kuu kuwa ushahidi yalikuwa ni maungamo yaliyopatikana kihalali kwa sababu yalionyesha vitu vinavyohusiana na mauaji kama vile silaha zilizotumika katika mauaji hayo, ambayo yalithibitishwa na ripoti za uchunguzi wa mwili wa marehemu ambazo ziliwasilishwa katika Mahakama Kuu. Mahakama hii pia iliona kwamba Mahakama ya Rufani pia ilitathmini kama ungamo la Mwombaji lilifanywa kwa hiari. Kuhusu madai ya utesaji, Mahakama ya Rufani ilikuwa na maoni kwamba Mwombaji hakumjulisha mlinzi wa amani kwamba aliteswa akiwa chini ya ulinzi wa polisi, na wala mlinzi wa amani hakuona michubuko wakati wa uchunguzi wa mwili wake. Mahakama ya Rufani ilihitimisha kuwa maelezo hayo hayakutolewa kwa mateso na kwamba yalikuwa ya kuaminika kama yalivyothibitishwa na ushahidi wa mlinzi wa amani mbele ya Mahakama Kuu.

Mahakama inabainisha zaidi kwamba Mahakama ya Rufani ilirejelea mamlaka yake, ambayo yanaitaka kuegemea kwenye ungamo iwapo hakuna uthibitisho, kunategemea masharti makali. Ambayo ni pamoja na, kuhakikisha kama maelezo yalitolewa kwa hiari, yalikuwa ya kuaminika na kama uthibitisho haukupatikana. Mahakama ya Rufani ilitumia vigezo hivi kwenye kesi inayomhusu Mwombaji na kujiridhisha kuwa Mwombaji alitiwa hatiani ipasavyo kutokana na ungamo alilotoa kwa hiari yake.

Hivyo, Mahakama iliona kwamba hakukuwa na chochote kwenye rekodi kuonyesha kwamba Mahakama ya Rufani ya Nchi Inayolalamikiwa ilimnyima Mwombaji fursa ya kupinga kutiwa kwake hatiani na hukumu yake. Mahakama ilihitimisha kwamba jinsi Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani iilivyoshughulikia maelezo ya Mwombaji yaliyotelewa nje ya mahakama na kuzingatia madai ya utesaji, havikuonyesha kutozingatiwa kwa viwango vilivyowekwa katika Mkataba.

Katika dai la pili linalohusiana na ukiukwaji wa haki za Mwombaji kutokana na kuchelewa kusikilizwa na kutolewa uamuzi wa maombi ya mapitio, Mahakama ilibaini kuwa Mwombaji alishindwa kutoa ushahidi kuwa Mahakama ya Rufani ilimpa kibali cha kuwasilisha maombi ya mapitio nje ya muda. Pia alishindwa kutoa ushahidi kwamba, baada ya kupewa ruhusa hiyo, aliwasilisha maombi ya mapitio hayo mbele ya Masjala ya Mahakama ya Rufani na kutoa taarifa kwa Nchi Inayolalamikiwa kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Kanuni za Mahakama ya Rufani. Kutokana na hali hiyo, Mahakama hii ilitupilia mbali madai ya Mwombaji na kubaini kuwa hakukuwa na ukiukwaji wa haki zake.

Dai la tatu la Mwombaji ni kwamba Nchi Inayolalamikiwa ilikiuka haki yake ya kujitetea kwa mujibu wa Ibara ya 7(1)(c) ya Mkataba kwa kushindwa kumpatia wakili wa chaguo lake. Mahakama ilirejelea Ibara

ya 7(1) (c) ya Mkataba, kama inavyosomwa pamoja na Ibara ya 14(3)(d) ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR), inamhakikishia mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kosa kubwa la jinai, haki ya kupewa wakili moja kwa moja bila malipo wakati wowote maslahi ya haki yanapohitaji hivyo, na kwamba hii inatumika kwa hatua zote za mashtaka na rufaa. Mahakama iliona kuwa Nchi Inayolalamikiwa ilimpatia Mwombaji uwakilishi wa kisheria bila malipo kwa gharama zake, kwa kutoa Mawakili watatu (3) ambao walimwakilisha katika hatua za kusikilizwa kwa kesi na rufaa. Mahakama pia ilibaini kwamba, hakuna chochote kwenye rekodi kilichoonyesha kwamba kulikuwa na pingamizi lolote lililowasilishwa mbele ya mahakama za ndani kuhusiana na kama Mawakili walitekeleza wajibu wao kwa kuathiri haki ya Mwombaji kujitetea. Hivyo, Mahakama ilibaini kuwa Nchi Inayolalamikiwa haikukiuka haki za Mwombaji chini ya Ibara ya 7(1)(c) ya Mkataba.

Ikijiridhisha kuwa Nchi Inayolalamikiwa haikukiuka haki za Mwombaji, Mahakama hata hivyo ilisisitiza kuhusu uamuzi wake katika kesi zake zilizopita kwamba adhabu ya kifo ya lazima ni ukiukaji wa haki ya kuishi miongoni mwa haki nyingine katika Mkataba na hivyo inapaswa kufutwa kwenye sheria za Nchi Inayolalamikiwa.

Kuhusu fidia, Mwombaji aliomba amri kwamba alipwe fidia kwa muda wa kifungo chake inayopimwa kwa kuzingatia "wastani wa kitaifa wa mapato ya raia kwa mwaka". Pia aliiomba Mahakama iamuru aachiliwe huru ili kurekebisha madhara aliyoyapata. Mahakama, baada ya kubaini kuwa hakuna ukiukwaji wa haki za Mwombaji uliothibitika, ilitupilia mbali maombi ya Mwombaji ya kulipwa fidia.

Kila Upande uliamriwa kubeba gharama zake.

Kwa mujibu wa Ibara ya 28(7) ya Protokali na Kanuni ya 70(1) ya Kanuni hizo, Jaji Blaise TCHIKAYA alitoa Maoni Tofauti kwa Sehemu fulani, Jaji Ben KIOKO, Jaji Tujilane R. CHIZUMILA na Jaji Dennis D. ADJEI walitoa Maoni Tofauti ya Pamoja na Jaji Chafika BENSAOULA alitoa Maoni Tofauti.

**<u>Taarifa zaidi</u>**

Taarifa zaidi kuhusiana na kesi hii, ikijumuisha nakala kamili ya uamuzi wa Mahakama ya Afrika, zinaweza kupatikana kwenye tovuti: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0312016

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Masjala kwa barua pepe: registrar@african-court.org.

Arusha, Tanzania
Tovuti: www.african-court.org
Simu: +255-27-970-430

**MUHTASARI WA HUKUMU**

*Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu ni mahakama ya bara iliyoanzishwa na Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika ili kuhakikisha ulinzi wa haki za binadamu barani Afrika. Mahakama ina mamlaka kuhusiana na kesi na migogoro yote iliyowasilishwa kwake kuhusu tafsiri na matumizi ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na hati nyingine yoyote muhimu ya haki za binadamu iliyoridhiwa na Mataifa husika. Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu: www.african-court.org.*